BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Saba – Tarehe 15 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

128. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Kwa kuwa imezoeleka kuwa vifungu vingi vya matumizi huingiziwa fedha kidogo kinyume na vilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, na kwa kuwa baadhi ya vifungu hutengewa

fedha nyingi kutokana na umuhimu wake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi zinapatikana kama zilivyopitishwa kwenye bajeti husika.

**<u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:</u>**

121. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kumekuwa na changamoto kubwa ya utekelezaji wa baadhi ya sheria zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi kutokana na kukosa kanuni za ufafanuzi wa Sheria hizo.

(a) Je, ni mambo gani yanayokwamisha kutungwa kwa kanuni hizo.

(b) Kwanini Serikali isitoe toleo au waraka kwa waheshimiwa Mawaziri na Wakuu wa Taasisi zake zitakazoainisha muda wa ukomo wa kutayarishwa kwa kanuni zinazotakiwa kutungwa kwa mujibu wa sheria zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(c) Kwanini Serikali haianzishi utaratibu wa kuleta miswada ya sheria Barazani ikiwa ni pamoja na kanuni zake zikiwa tayari zimeshatayarishwa.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

95. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kuwepo kwa mikutano ya kila mwezi ya Mheshimiwa Rais na waandishi wa habari ni jambo jema. Hata hivyo, tathmini ya wananchi wengi ni kwamba, mikutano hiyo inawanyima fursa Mawaziri na Wakuu wengine wa Taasisi za Serikali, katika kutekeleza mipango ya Wizara na Taasisi hizo kibajeti, kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi. Hali hii inatokana na kulazimika kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais ambayo kwa kiasi kikubwa hayako kwenye mipango ya mwaka ya Wizara au Taasisi husika.

(a) Je, ni upi mtazamo wa Serikali kuhusu utaratibu huu ambao unaonekana kuwanyima fursa za kutekeleza

mipango ya kibajeti kwa Wakuu wa Wizara na Taasisi zake.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kurasimisha maagizo ya Mheshimiwa Rais ambayo ni mengi na yanahitaji bajeti ya ziada ambayo haikupangwa kwa mwaka husika.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

145. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika safari za ndege kupitia kampuni ya ndege ya Unity Air, kumekuwa na tabia ya ubadilishaji wa mizigo ya abiria wanaotoka Unguja kwenda Pemba pale ambapo ndege mbili zimekuja kwa wakati mmoja. Jambo hili linawaletea usumbufu mkubwa abiria .

(a) Je, kwa kiwango gani Mheshimiwa Waziri unalitambua tatizo hili.

(b) Je, ni nini hasa sababu ya kutokea kwa hali hii.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

65. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Shirika la umeme linaendelea na kazi ya kupeleka umeme katika kijiji cha Kivumoni kilichopo shehia ya Mtambwe Kusini na muda mrefu sasa kazi hiyo imesimama.

Je, sababu zipi zilizopelekea kusimama kwa kazi hiyo na wananchi wameshajenga matumaini ya kupata huduma hiyo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

29. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Wananchi wa Shehia za Kilimani Chuini na Kama wanategemea uvuvi katika kuendesha maisha yao na wameendelea kuwa na matumaini makubwa ya kufaidika kutokana na kuwepo kwa Wizara hii, kwa kuimarishiwa maeneo ya masoko ya samaki, dagaa na kupatiwa vyombo vya uvuvi.

(a) Katika mpango wa Serikali wa kutoa boti kwa vikundi vya ushirika Je, ni vikundi vingapi kutoka jimbo la Mfenesini vinatarajiwa kupata boti hizo.

(b) Ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya bandari ya kuuzia dagaa shehia ya Kihinani na Kama.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

5. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali imeahidi kutoa miche 500,000 ya mikarafuu na miche 500,000 ya minazi kwa kipindi cha 2021/2025.

Je, hadi sasa ni miche mingapi ya minazi na miche ya mikarafuu iliyotolewa bure kwa wananchi ili kuimarisha kilimo hicho hapa nchini.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

96. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu utaratibu, nyenzo, muda wa uhakiki wa Pencheni ya Jamii na wanufaika wake.

(a) Je, ni upi utaratibu wa sasa juu ya uhakiki huo wa Pencheni ya Jamii na tathmini yake ikoje.

(b) Je, ni mpango upi wa Serikali wa kuboresha zoezi hilo ili wale wote wanaostahiki kupata haki wapate haki hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

41. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wananchi wa Shakani – Buyu wanapata tabu katika kupata huduma ya elimu kwani wanafunzi wanaoishi katika maeneo hayo hutembea zaidi ya kilomita nne na nusu kwenda skuli. Hali hii inaongeza matukio ya udhalilishaji dhidi ya wanafunzi hao, lakini pia uchovu na kupunguza kiwango cha ufaulu wa

wanafunzi hao.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuanza ujenzi wa skuli kwa upande wa Shakani – Buyu.

(b) Je, ni lini ujenzi wa skuli hiyo katika eneo la Shakani-Buyu utaanza ili kuondoa changamoto kwa wanafunzi hao.

**Wizara ya Afya:**

56. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi yasiyo ya kuambukiza (NCD) kama vile kisukari na pressure hapa nchini petu, ambayo pamoja na sababu nyengine yamekuwa yanaongezeka kwa tabia ya Wanzanzibari (walipa kodi) kushindwa kuwa na utaratibu wa kwenda hospitali pamoja na vituo vya afya kupima afya zao na hivyo kuathiriwa kwa hali ya juu na magonjwa haya nyemelezi.

Je, ni lini Serikali kupitia Wizara yako itaanzisha utaratibu wa Maabara Tembezi (Mobile Doctors and Laboratory), kwa ajili ya kupita vijijini na kuwafanyia vipimo walipa kodi wa nchi hii ili kupunguza athari ya maradhi haya sugu.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

Ripoti ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**15 Septemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**